REPOA *Muhtasari*

www.repoa.or.tz RESEARCH ON POVERTY ALLEVIATION

Muhtasari 7
Februari
2008

# Mawazo ya AZISE za Tanzania Kuhusu Uhusiano Wao na Serikali

Kutokea miaka ya 1980, dhima ya jamii za kiraia katika maendeleo ya Tanzania na huduma za jamii imepanuka sana, na idadi ya Asasi Zisizo za Kiserikali (AZISE) imeongezeka kwa haraka sana kutoka asasi 17 tu zilizosajiliwa mwaka 1978, hadi maelfu ya AZISE zinazofanya kazi Tanzania sasa.

Kwa kutambua umuhimu wa sekta hii, serikali ya Tanzania ilipitisha Sheria ya AZISE, 2002. Sheria hii ilitungwa kuweka wazi uhusiano kati ya serikali na AZISE, na kuziwezesha AZISE kufanya kazi kwa ufanisi zaidi kote nchini.

Lakini je hali imekuwa bora? AZISE zinaweza kufanya kazi kwa uhuru Tanzania? Au kuna mabadiliko na maboresho zaidi yanahitajika?

Kujibu maswali haya, mwaka 2005 REPOA kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Dublin City walitafiti AZISE 91 za Tanzania kupata mawazo yao kuhusu mazingira ya AZISE katika Tanzania ya leo.

AZISE za mijini na vijijini kwenye mikoa 8 kati ya 26 ya Tanzania zilihusishwa. Washiriki waliulizwa kuhusu dhima ya asasi zao pamoja na uhusiano baina yao na serikali na wafadhili.

Kutia mkazo mambo ambayo AZISE wanasema, REPOA imeandaa mihutasari miwili. Muhtasari huu wa kwanza unaelezea mawazo ya AZISE kuhusu uhusiano wao na serikali. Muhtasari wa pili utaeleza zaidi mawazo kutoka kwa AZISE kuhusu uhusiano wao na wafadhili.

Kwa ujumla washiriki walitoa taarifa kuwa uhusiano huu unaimarika pamoja na mazingira ya AZISE kufanya kazi ya kwa ujumla. Hata hivyo, waliotoa baadhi ya mapendekezo muhimu kuhusu jinsi mambo yanavyoweza kuboreshwa ili AZISE, serikali na wafadhili waweze kufanya kazi kwa pamoja kufikia maelengo ya pamoja ya kupunguza umaskini na kuinua hali ya maisha ya Watanzania wote.

### Uhusiano wa AZISE – Serikali

Kwa ujumla, washiriki waliashiria kuwa uhusiano baina ya AZISE na serikali ya Tanzania unaboreka, ukionyeshwa na mawasiliano yanayoongezeka, kuchangamana na kuaminiana kati ya makundi haya mawili. Serikali inatafuta habari na ushiriki zaidi wa AZISE. Waliojibu maswali pia walihisi kuwa serikali sasa ina uelewa mzuri zaidi wa dhima muhimu ya jamii za kiraia katika kuunda sera. Hata hivyo, hali ya mashaka bado ipo, na baadhi ya AZISE wana wasiwasi kama kweli serikali inatoa taarifa zake bila vizuizi.

Maoni haya mchanganyiko yanajitokeza katika maneno ya mshiriki mmoja:

> *"Serikali inaanza kutuelewa sisi [AZISE] vizuri, inaanza kuangalia kazi zetu, kwa kuona wapi tunaweza kuwa wa manufaa kwao, nini nguvu zetu na udhaifu wetu. [Lakini] sehemu fulani za serikali zinatutaka sisi tuwe nje, wakati zingine zinatuogopa zaidi. Zingine zinathamini mchango wetu; zingine zinatutenga."*

### Dhima ya AZISE

Licha ya hali ya kuaminiana inayokua, AZISE zinaamini kuwa wananchi na jamii za kiraia lazima waendelee kupima na kufuatilia kwa karibu utendaji wa serikali. Kwa maneno mengine, jamii za kiraia zina dhima inayoendelea kama 'waangalizi' ili kulinda 'maslahi yao ya kijamii'. Kama mhojiwa moja alivyosema:

> *"AZISE lazima ziwe mstari wa mbele katika kuchambua sera na mikataba ya serikali."*

Vile vile, AZISE zinaweza kusaidia kuimarisha sera na mipango ya serikali. AZISE zina ufahamu na ujuzi wa jamii zao. Zinaweza kupitisha na kufasiri taarifa kutoka na kwenda kwenye jamii na serikali, na zinaweza kupendekeza na kutekeleza suluhu bunifu kwa matatizo ya jamii. AZISE pia ziliainisha dhima yao muhimu katika utoaji wa huduma, pale ambapo serikali haina au ina upungufu wa uwezo wa kutoa huduma muhimu za kijamii.

Kwa kweli, shughuli za karibu theluthi mbili (62%) ya AZISE zilizotafitiwa zilihusisha utoaji wa huduma; kazi za zaidi ya theluthi mbili (68%) za asasi zilihusisha ushawishi, na karibu robo (21%) ya asasi walijihusisha katika ngazi mbali mbali za utafiti. Tatu ya tano (60%) ya asasi zilizotafitiwa pia zilijipanua maeneo ya kazi ili kujibu mahitaji yanayobadilika ndani ya jamii zao, na zaidi ya 80% ya AZISE zilisema kuwa shughuli za ushawishi zimekuwa muhimu zaidi.

### Kuifikia Serikali

Karibu AZISE zote zilizoshiriki kwenye utafiti zilikuwa na uhusiano wa moja kwa moja na serikali, kama asasi binafsi, kupitia mitandao au kwa kutumia njia zote mbili. Karibu nusu ya asasi hizi ziliwasiliana na ngazi zote za serikali – taifa, mikoa, wilaya, kata na kijiji – wakati takriban, theluthi moja hufanya hivyo katika ngazi ya wilaya tu. Zaidi ya 40% ya AZISE zilikuwa zinawasiliana na maofisa wa serikali kila mwezi au kwa robo mwaka. Karibu 30% zilikuwa na mawasiliano ya kila siku au kila wiki. Hata hivyo, karibu theluthi moja ya waliojibu maswali walisema kuwa mawasiliano kati yao na serikali yalikuwa ni kwa matukio maalum tu.

Kwa ujumla, zaidi ya 60% ya AZISE zilielezea kuwa kiwango chao cha mawasiliano na serikali kinatosheleza. Hata hivyo, matokeo ya utafiti yanaashiri kuwa vikundi vya vijijini vinawasiliana kwa kiasi kidogo sana na zinakabiliwa na vipingamizi vingi kuifikia serikali ukilinganisha na AZISE za mijini. AZISE nyingi za vijijini hazina fursa za kushiriki kwenye mikutano ya watunga sera kwa ngazi za juu Dar es Salaam. Hatua za kuboresha sauti za asasi ndogo za vijijini zinapaswa kuanzishwa, ili jamii za kiraia zisiwe za Dar es Salaam peke yake.

### Athari kwenye Upunguzaji Umaskini na Maendeleo

Karibu robo tatu ya washiriki waliamini kuwa asasi zao zilikuwa na athari 'kubwa' au 'wastani' katika kupunguza umaskini na kuleta maendeleo Tanzania, na wengi walitoa kwa mfano kazi zilizofanikiwa za AZISE kubwa. Hata hivyo, asasi nyingi zilitathmini athari zao kwa kuzingatia maelezo na mitazamo ya mabadiliko, na chini ya moja ya tano ya waliojibu maswali walitumia njia rasmi za kusimamia na kutathmini ili kupima ufanisi wao. Wengine walihisi kuwa mabadiliko halisi machache tu yanaweza kupimwa kwa sasa.

Kwa ujumla, athari chanya zilizoelezwa ni za muhimu na kutia moyo, lakini kwa sehemu kubwa ni ya jamii husika na haziwezi kuchukuliwa kama mafanikio ya kitaifa.

Hata hivyo, AZISE pia zimeeleza mchango wao unaokua katika utungaji wa sera, na jitihada hizi zina wigo mpana.

### Athari kwenye Sera za Serikali

Washiriki wote wa utafiti, kasoro mmoja, walihisi kuwa AZISE zinaathiri sera za serikali. Eneo lililotajwa mara nyingi kuathiriwa na shughuli za AZISE kwenye sera ni mchango wao kwenye kupitia Mkakati wa Kupunguza Umaskini (PRS), mchakato serikali wa mashauriano ya kitaifa kwa ajili ya MKUKUTA, mkakati wa Tanzania wa miaka 5 wa ukuaji na kupunguza umaskini.

Washiriki walihisi kuwa mapendekezo yao mengi yalijumuishwa kwenye MKUKUTA katika sehemu kama za ulemavu, usawa wa jinsia na vyanzo mbadala vya nishati. Waliojibu maswali walisema kuwa mchakato wa PRS umesaidia sana kujumuisha vita dhidi ya umaskini katika sera za serikali na kutengeneza utambuzi mpya nchini kwamba umaskini si hali ya kawaida na inaweza kuondolewa. AZISE nyingi zilichangia mada kwenye masuala ya jamii na kushiriki kwenye warsha - ishara inayotia moyo sana kwa jamii za kiraia kwa ujumla. Mawazo haya chanya yalielezwa katika nukuu ifuatayo:

> *"Ndiyo, serikali imejielekeza kwenye MKUKUTA, nayo ni athari kubwa. Kwamba serikali imejipanga upya kwa kiasi hicho ni hali pekee kwa Tanzania; inayoweza kuwa sababu wafadhili wanaielezea vizuri Tanzania. Na kwa baadaye, ilani ya CCM pia imejipanga katika MKUKUTA."*

Washiriki wengine walikuwa na wasiwasi. Hawakuona matokeo ya wazi kutoka kwenye mchakato wala ongezeko la rasilimali kwenye huduma za jamii. Mshiriki mmoja alielezea mchakato wa PRS kama *"makaratasi, siasa na utaratibu wa fedha kuhusu nani anapata nini, lakini siyo nyenzo ya maendeleo."*

AZISE zilionyesha michango mingine iliyofanikiwa katika eneo la mabadiliko ya sheria – mageuzi ya ardhi, elimu, mambo ya vijana, na mikakati ya kupunguza deni la taifa – lakini pia walionyesha vipingamizi walivyokumbana navyo katika kushawishi sera. Asasi moja isiyo ya kiserikali ilisema kuwa serikali husikiliza hoja kali na nzito, lakini ikaongezea kuwa ushawishi unachukua muda mrefu sana, na kwamba ilikuwa ngumu kuifanya serikali kusikiliza. Kwa kweli, kulikuwa na maoni ya ujumla kutoka kwa washiriki kuwa kama taarifa hazikukubaliana na msimamo wa serikali au kama maslahi ya msingi yamepingwa, basi juhudi za AZISE zitakuwa na athari ndogo au hazina athari kabisa. Mawazo haya yanaashiria kuwa ili kufikia ushiriki mpana na wenye ufanisi wa jamii za kiraia, mazingira ya uandaaji sera yanahitaji kufunguliwa.

### Jinsi Gani AZISE Zinaweza Kushawishi Sera kwa Ufanisi?

Washiriki walikubaliana kwamba jitihada zozote za ushawishi zinapaswa kuwa na taarifa na maandalizi ya kutosha. Kuitazama serikali kama adui pia ilionekana kuwa kikwazo. Hasa, AZISE ziliweka wazi kuwa hali ya kukubaliana, wakipendekeza kuungana na kushirikishana zaidi na serikali.

Ili kushawishi kikamilifu mijadala ya sera, AZISE zinahitajika kufanya 'maandalizi' yao kabla na kuainisha mahali na muda muafaka wa kushiriki. Asasi lazima ijua kabla masuala vizuri pamoja na msimamo wa serikali dhidi yake. Kisha maofisa husika katika ngazi zinazofaa wanaweza kupewa mapendekezo kwa njia ya wazi na hoja zenye kushawishi.

AZISE nyingi zilishawishi kuchukua hatua ya pamoja katika kuleta masuala mbele ya serikali. Kwa kweli, baadhi ya waliojibu maswali walipendekeza kuwa kutokuwepo kwa umoja miongoni mwa AZISE katika masuala muhimu ni udhaifu kwa jamii za kiraia za Tanzania. Kama AZISE hazijaunganisha sauti zao vizuri kwa harakati za pamoja, watakuwa 'wanapiga kilele hewani.' Kwa hiyo, waliona kuwa mitandao na muungano kuwa ni muhimu sana katika kuendeleza sera zinazowajali maskini. Makundi haya huruhusu taarifa na ujuzi kutumniwa kwa pamaoja, na kutoa uaminifu mkubwa zaidi kwa AZISE zinazoshawishi serikali. Mitandao pia inaweza kusaidia kuziunganisha AZISE kufanya kazi pamoja kwa shughuli zilifadhiliwa kwa pamoja.

**Jinsi Gani Serikali itawezesha Kazi za AZISE?**

Zaidi ya kuimarisha uwezo na ushirikiano wao wenyewe, AZISE zinazoshiriki pia zilipendekeza njia mbalimbali za serikali kuwawezesha kazi zao. Serikali ilenge:

- Kujenga ubia na jamii za kiraia ili kushinda ukinzani wowote wa 'sisi na wao' na kuwezesha ushirikiano kwa malengo ya pamoja;
- Kuweka njia wazi za mawasiliano kati ya serikali na jamii za kiraia;
- Kuongeza upatikanaji wa taarifa za serikali kwa kutokufungia taarifa, uwazi na uwajibikaji;
- Kujaribu dhana ya kugharamia miradi ya pamoja katika maeneo ya vipaumbele vya MKUKUTA – njia ya kushikamana zaidi kuliko matokeo ya jitihada binafsi AZISE ndogo ndogo nyingi zinazofanya kazi kwa kujitenga;
- Kunganisha AZISE zenye mwelekeo sawa na ujuzi unaofanana kufanya kazi kwenye miradi ya pamoja inayogharamiwa na serikali au wafadhili;
- Kutoa fedha na/au rasilimali kwa AZISE, hii ikiwa ni pamoja na mafunzo, msaada wa kiufundi na kuwajengea uwezo; na
- Kupitia Sheria ya AZISE kuruhusu AZISE kufanya kazi kwa uhuru zaidi na kwa ufanisi, na hapo kuweka mazingira wezeshi ya kisiasa kwa jamii za kiraia.

**Hitimisho**

Katika utafiti mzima, AZISE ziliwasilisha kwa dhati na ukweli, na kuelezea matamanio yao ya wazi kwa ubia wa kweli na serikali na mawakala wa wafadhili. Waliojibu maswali walionyesha kuwa wakati wafadhili na serikali wanaweza kuwa na fedha, ni AZISE ambazo zina uzoefu na ujuzi wa shughuli za jamii zao. Kwa hiyo, kwa kufanya kazi pamoja kama wabia halisi – kwa kuwahusisha AZISE katika kutunga na kupanga sera na mipango, kwa kupunguza urasimu na kwa kuzingatia vipaumbele vya AZISE badala ya ajenda za kiimla – mengi zaidi yanaweza kufanywa kuelekea malengo ya pamoja ya kupunguza umaskini na kuongeza maendeleo Tanzania. Kama mshiriki mmoja alivyofafanua dhahiri:

*"[Sekta zote mbili] zinawatumikia watu hao hao – raia wa Tanzania."*

---

Muhtasari huu unatoa taarifa kutoka ripoti ya AZISE za Tanzania – Mawazo kuhusu Uhusiano wao na Serikali ya Tanzania na Wafadhili, na Dhima na matokeo katika Kupunguza Umaskini na Kuongeza Maendeleo Tanzania.

Ripoti hii inapatikana kwa nakala pepe kutoka: **www.repoa.or.tz**

Maktaba ya REPOA inafunguliwa saa 4.00 mpaka 7.00, na 8.00 mpaka 11.00 siku za Jumanne hadi Ijumaa.

**Kwa kupata taarifa zaidi kuhusu machapisho mengine ya REPOA wasiliana na:**

**Research on Poverty Alleviation (REPOA)**
**157 Mgombani Street, Regent Estate**
**S.L.P. 33223**
**Simu: (022) 270083**
**Nukushi/Faksi: (022) 2775738**
**Barua pepe: repoa@repoa.or.tz**
**Anwani ya tovuti: http://www.repoa.or.tz**

**ISBN: 978-9987-615-18-6** **© REPOA 2008**